

**KIDATO CHA TATU
KARATASI YA 102/2
KISWAHILI
MTIHANI WA MWISHO WA MUHULA - MACHI 2014
MUDA: SAA 2 ½**

JINA:.....NAMBA RI YA USAJILI:.....

DARASA:TAREHE:.....

Maagizo:

- (a) Karatasi hii ina sehemu A, B, C, D na E.
- (b) Jibu maswali yote katika karatasi hii.
- (c) Majibu yote kwenye sehemu uliyopewa pekee.
- (d) Makose yote ya sarufi na hijai yataadhibiwa.

Kwa matumizi ya mtahini pekee

SEHEMU	MADA	UPEO	TUZO
	UFAHAMU	15	
	SARUFI	40	
	ISIMU JAMII	10	
	KIDAGAA KIMEMWOZEA	20	
	SHAIRI	15	
	JUMLA	100	

Ufahamu

Umaskini Afrika

'Mwenyekiti wa Kamati Andalizi ya kongamano hili, mabibi na mabwana. Umaskini ndilo tatizo kubwa zaidi barani Afrika. Je, maana yake halisi ni nini? Umaskini ni ile hali ya mtu kukosa chakula, makazi na uwezo wa kumiliki mali au kushiriki shughuli za kuzalisha mali. Nchini Kenya, mtu husemekana kuwa mkata iwapo pato lake ni chini ya shilingi 1,239 kwa mwezi. Umaskini umetopea barani Afrika kiasi kwamba 60% ya wakazi wake wametota katika dimbwi la uchochole. Dhiki kubwa ya hali hii inapatikana majijini ambamo wengi wanaishi katika mitaa ya mabanda.

Kuna mambo mengi yanayochangia kuwepo umaskini. Moja ya mambo haya ni kuongezeka kwa idadi ya watu. Hivi sasa, kuna Waafrika milioni 800, wakiwemo Wakenya milioni 29. Jambo la pili, ni kuwa chumi zimeporomoka na mapato ya kitaifa ya nchi nyingi yamedidimia. Kwa hivyo, serikali zinashindwa kutoa huduma za kimsingi kama chakula, maji na afya kwa raia. Ili kujiokoa, nchi nyingi zinaamua kukopa kutoka nchi zilizoendelea. Baadaye, nchi za Kiafrika hulazimika kutumia fedha kidogo zinazopata kulipia riba huku wananchi wakiteseka. Hivi ninapozungumza, Bara la Afrika lina deni la dola bilioni 300. Kati ya hizi, Kenya inadaiwa dola bilioni saba.

Bwana mwenyekiti, jambo la tatu lichangialo ufakiri ni masharti yanayoambatana na mikopo. Nchi nyingi zimelazimishwa kuweka soko huru, kubinafsisha mashirika ya umma na kupunguza idadi za wafanyakazi. Matokeo ni kuwa bidhaa kutoka nje zinaangamiza viwanda. Tena nafasi za ajira sasa ni finyu hata vijana wenye shahada za vyuo vikuu leo wanasaga lami mitaani kutafuta kazi.

Umaskini Afrika pia unatokana na bei duni ya masoko ya nje. Bara la Afrika limekuwa likiuza rasilimali na mazao kwa nchi zilizoendelea kwa bei ya kijungu jiko. Hivyo, nchi za Afrika hazipati faida za kuweza kuimarisha hali ya maisha ya watu wake. Isisahaulike kuwa sisi wenyewe tunachangia umaskini. Hii ni kutookana na uongozi mbaya. Mipango ya maendeleo ya watawala wengi ni mibaya. Mfano wa hii ni ubadirifu wa pesa kwa miradi ya fahari kama viwanda vya silaha ambavyo havina faida kwa raia.

Utawala mbaya husababisha masumbuko, chuki na uadui ambaou huchochea migogoro na vita vya sisi kwa sisi. Jambo hili husababisha sio tu uharibifu wa mali na mazingira, lakini vifo vya Waafrika wengi. Bila amani, shughuli za kuinua uchumi hukwama.

Sote twafahamu uovu wa rushwa. Lakini katika nchi nyingi za Kiafrika, ujisadi umejisimika vilivyo. Rasilimali ambazo zingewafaidi wote, huporwa na kunufaisha vigogo wachache tu na vibaraka wao. Aidha majanga mengine husababisha umaskini. Baadhi ya haya ni matukio ya kimaumbile kama vile mafuriko, ukame na mitetemeko ya ardhi. Matukio haya huangamiza watu na kuharibu mali na miundo msingi kama barabara. Hivi sasa, bara letu linakabiliwa na tisho kubwa; Ukimwi. Kila siku watu takriban 20,000 wanapoteza maisha. Pesa nyingi zimetumiwa kugharamia matibabu, mazishi na kutunza mayatima.

Mabibi na mabwana. Umaskini ni ugonjwa mbaya. Unapotokea, husambaa na kusababisha matatizo mengine mengi. Ulevi, uasherati, mauaji, uhalifu, uombaraji, maradhi, matumizi ya dawa za kulevyo, uchafuzi wa mazingira, na kadhalika, ni matokeo ya umaskini. Swali kuu ni: je, tufanye nini ili tujiondoe kwenye makucha makali ya umaskili?

- (a) Toa kichwa mwafaka kwa taarifa uliyosoma. (al 2)

.....

- (b) Kulingana na taarifa umaskini ni nini? (al 2)

.....

- (c) Fafanua mambo matatu yanayosababisha umaskini barani Afrika. (al 3)

.....

.....

.....

.....

.....

.....

- (d) Eleza umuhimu wa mikutano ya kujadili umaskini. (al 2)

.....

.....

.....

- (e) Taja athari zozote nne za umaskini kama anavyoeleza mwandishi. (al 4)

.....

.....

.....

- (f) Fafanua maana ya: (al 2)

(i) Wametota katika dibwi la umaskini -

.....

(ii) Wanasaga lami -

.....
SEHEMU B: (ALAMA 30)

SARUFI

- (a) Nini maana ya silabi fungo? Toa mfano. (al 2)

Maana:

.....
.....

Mfano:

- (b) Kwa kutolea mfano mwafaka., eleza maana ya mofimu huru. (al 2)

.....
.....
.....
.....

- (c) Kwa kutolea mfano moja moja, eleza maana ya ala zifuatazo. (al 2)

(i) Ala tuli

.....
.....

(ii) Ala sogezi

.....
.....

- (d) Tunga sentensi yenye viungo vifuatavyo:

(i) Kiambishi kiwakilishi cha nafsi ya tatu umoja. (al 2)

.....
.....

(ii) Kiambishi kiwakilishi cha wakati uliopita. (al 2)

.....
.....

(iii) Mzizi wa kitenzi (al 2)

.....
.....

(iv) Kiishio (al 2)

.....
.....
.....
(e) (i) Nini maana ya kivumishi. (al 2)

.....
.....
.....
(ii) Toa mfano wa kivumishi kiashiria katika sentensi. (al 2)

.....
.....
(f) Bainsiha vitenzi katika sentensi ifuatayo. (al 2)

Fisi anaonekana anachechemea

.....
.....
.....
.....
.....
(g) Andika sentensi ifuatayo upya katika hali iliyoonyeshwa katika mabano. (al 2)

Nilikula kishuka murua jana alasiri (tendeshwa)

.....
.....
.....
(h) Alama zifuatazo za uakifishi zimetumiwa kuleta dhana gani? (al 2)

I. Madereva (wa matatu) wamepata leseni

II. Nilizaliwa mwaka wa '57.

(i) Yakinisha sentensi ifuatayo. (al 2)

Naliaka hakununua kitabu

.....
.....
.....
(j) Tunga sentensi kubainisha kundi tenzi na kundi nomino. (al 2)

(k) Unda nomino kotokana na nomino zifuatazo. (al 2)

(i) Mpambe

(ii) Mkalimani

(l) Changanua sentensi ifutayo kwa njia ya mchoro wa matawi. (al 4)

Fundi hodari ametujengea nyumba.

.....
.....
.....
.....
.....

(m) Andika kwa usemi halisi. (al 3)

Mama alituambia kuwa tungeenda sokoni asubuhi ya siku iliyofuatia.

.....
.....

SEHEMU C (ALAMA 10)

ISIMU JAMII

1. ...beba! Beba! Bebaa! Come sister....bei nafuu...

(a) Tambua sajili hii. (al 1)

.....

(b) Eleza sifa tatu za sajili hii. (al 3)

.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

2. Eleza sifa tatu za sajili ya vijana. (al 3)

.....
.....
.....
.....
.....
.....

3. Kwa mujibu wa katiba ya Kenya, Omukofu umevunja sheria ya

- (a) Tambua sajili hii. (al 1)

.....
.....

- (b) Eleza sababu mbili za kutumia lugha yenye sifa zinazojitekeza katika dondoo hili.
(al 2)

.....
.....

SEHEMU D: (ALAMA 20)

Kidagaa Kimemwozea

- (a) Uchochole umewakumba wananchi wengi wa sokomoko. Dhibitisha kwa kutoa mifano
yoyote mitano. (al 10)

- (b) Kwa kuzingatia mifano yoyote mitano eleza matumizi ya majazi katika Kidagaa
Kimwemwozea. (al 10)

SEHEMU E: (ALAMA 15)

SHAIRI

Kiumbe kuwa makini, kwa jambo usolijua,
Kujitia hamkani, kuhangaika na juu,
Utangia fedhehani, na kubaki kujutia,
Kwa jambo usolijua, kweli usiku wa giza.

Acha yako masikio, kuyakisiya ya watu,
Kutegeza masikio, kusikiza wathubutu,
Kuyawacha ulonayo, kutwa fyaratu fyaratu,
Kweli usiku wa giza, kwa jambo usolijua.

Jii

Kama jambo hulijui, si lazima kulisema,
Uzushi haukufai, hauna hatima njema,
Bora utafute rai, ikwepushie nakama,
Bure wajisumbua, kwa jambo usolijua.

Nyamaza kimya

1. Lipe shairi hili kichwa mwafaka. (al 1)

.....

.....

2. Taja na udhibitishe bahari zozote katika shairi hili. (al 6)

.....

.....

Digitized by srujanika@gmail.com

Digitized by srujanika@gmail.com

.....

3. Eleza mbinu za lugha zilizotumina na mwandishi. (al 6)

4. Onyesha mpangilio wa vina na mizani katika ubeti wa tatu. (al 2)

.....
.....
.....
.....